# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

MADA KUHUSU

# "MIGOGORO KATIKA NCHI ZA AFRIKA NA DEMOKRASIA"

ILIYOTOLEWA NA

DR. SALIM AHMED SALIM
MWENYEKITI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE

KWENYE KONGAMANO LILILOANDALIWA NA
ZANZIBAR PRESS CLUB

AFRICA HOUSE HOTEL
ZANZIBAR
31 JULAI 2004

*Mada kuhusu*
***"Migogoro katika nchi za Afrika na Demokrasia"***
*iliyotolewa na Dr. Salim Ahmed Salim*
*Kwenye Kongamano lililoandaliwa na Zanzibar Press Club*

Ndugu Viongozi na wanachama wa **Zanzibar Press Club,**

Ndugu Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa **Zanzibar Press Club** kwa kunialika katika Kongamano hili na kunipa fursa hii adhimu ya kuwa msemaji mkuu wa mada hii muhimu ambayo inahusu amani, utulivu na maendeleo ya Bara la Afrika. Katika kufanya hivyo nitajaribu pia kutumia uzoefu nilioupata nikiwa mtumishi mkuu wa Bara letu kwa muda wa miaka kumi na mbili mfululizo.

Napenda pia kutoa pongezi kwa **Zanzibar Press Club** kwa kuandaa kongamano kama hili ambalo litatupa nafasi ya kuzingatia na kubadilishana mawazo kuhusu hali ya migogoro katika nchi zetu mbali mbali za Afrika na pia maendeleo na matatizo ya kuandaa au kuimarisha misingi ya kidemokrasia. Umuhimu wa kujadili mambo haya hautokani tu na ukweli kwamba bara letu limepatwa na linaendelea kukumbwa na maafa na misukosuko mikubwa kutokana na migogoro hiyo. Lakini ni vyema pia tukaelewa na kujifunza yale mambo yaliyosababisha migogoro hiyo ili nasi tuhakikishe kwamba tunaepukana na dosari za wenzetu na kwa upeo huo tuepukane na mambo na/au vitendo ambavyo vinaweza kuathiri au kutishia amani na utulivu katika taifa letu.

Waandishi wa habari kwa jumla yao wana majukumu makubwa katika taifa lolote lile lakini hasa lile lenye lengo la kujenga utawala wa uwajibikaji kwa wananchi wake. Vyombo vya habari ni mojawapo ya nguzo nne muhimu za dola (*The Fourth Estate*) la kisasa. Ni matumaini yangu kwamba wanachama wa **Zanzibar Press Club** na waandishi wa habari wa Tanzania kwa jumla watakuwa mstari wa mbele katika ubunifu na uadilifu ili kufanikisha wajibu huo. Natoa ushauri huo nikiwa mwenzenu wa zamani. Kwani nami nilipokuwa kijana wa miaka ishirini na ishirini na moja kabla sijaenda kuwa Balozi wa Zanzibar na hatimaye wa Tanzania huko Misri, nilikuwa mwandishi wa habari na pia kushika nafasi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Waandishi wa Habari wa Zanzibar (*All Zanzibar Journalists Organisation*).

Baada ya kusema hayo, sasa nirejee kwenye mada iliyotukasanya sote hapa. Nianze na historia kidogo. Nchi za Afrika, ukiwacha Ethiopia, Misri na Liberia zilikuwa chini ya ukoloni wa namna moja au nyingine. Nyingi miongoni mwa nchi hizi zilijipatia Uhuru wake bila ya umwagaji wa damu. Lakini, nyingine kama vile Algeria, Angola, Guinea Bissau, Kenya, Msumbiji, Namibia, Zimbabwe na hata Afrika ya Kusini zililazimika kuwa na mapambano ya silaha ya muda mrefu.

Maelfu kwa maelfu ya wananchi walijitolea mhanga ili kufanikisha lengo la ukombozi. Kwa mfano, katika vita vya ukombozi wa Algeria dhidi ya utawala wa kikoloni wa Kifaransa wananchi milioni moja waliuawa na wengi zaidi kupata vilema, vingi vikiwa vya maisha! Katika vugu vugu hilo la ukombozi, viongozi wetu mashuhuri kadhaa waliuawa kikatili. Miongoni mwao ni Patrice Lumumba wa Congo, Felix Moumie wa Cameroon, Eduardo Mondlane wa Msumbiji na Amilcar Cabral wa Guinea Bissau ambayo wakati ule ilikuwa iko pamoja na Cape Verde.

Athari nyingine kubwa ya mapambano haya baina ya wapigania uhuru na watawala wa kikoloni ni kuzuka kwa maelfu kwa maelfu ya wananchi waliolazimika kukimbia makwao na kuwa wakimbizi katika nchi jirani. Tanzania ina uzoefu mkubwa wa jambo hili kwani licha ya kuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi huru za Afrika, tuliwapokea na kuwahifadhi ndugu zetu wengi kutoka nchi mbali mbali ambako mapambano yalikuwa yamepamba moto.

Jambo moja kubwa lilisaidia kufanikisha juhudi za watu wetu kupambana na ukoloni na utawala wa makaburu. Nalo ni umoja na mshikamano. Ilikuwa ni hivyo katika zile nchi ambazo zilipigania uhuru bila ya kulazimika kuchukua silaha na hivyo hivyo kwa zile nchi ambazo vyama vya ukombozi vililazimika kuendesha mapambano kwa kutumia mitutu ya bunduki. Kutokana na historia hii tungetegemea kuwa baada ya uhuru na ukombozi, nchi zetu zingeimarisha

umoja na mshikamano na kutumia muda wake, nguvu zake na rasilmali zake pamoja na nguvu kubwa ya watu wetu katika kuleta maendeleo. Pia tungetegemea kuwa tusingekubali kabisa tofauti zetu ndogo ndogo kuachiwa zikakua, kuleta mfarakano katika jamii na kukuzwa zikawa migogoro mikubwa kufikia kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe – hali ambayo imeleta janga kubwa katika bara letu na hapo hapo kuwafadhaisha marafiki zetu na kuwafurahisha wale wasiotutakia mema.

Ni ukweli usiofichika kwamba mojawapo ya changamoto kubwa inayokabili Bara la Afrika ni migogoro isokwisha iliyopo ndani ya baadhi ya nchi zetu. Na tukiweka upande vita vya hivi karibuni baina ya Ethiopia na Eritrea – vita ambavyo vimetushangaza na kutuhuzunisha wengi hasa ukizingatia historia na uhusiano wa karibu sana wa kifamilia ya mataifa haya mawili – migogoro mingine yote iliyosambaa katika bara letu inatokana na matatizo ya ndani ya nchi. Orodha ni ndefu ingawa kumekuwa na maendeleo ya kutia moyo katika kutanzua baadhi ya migogoro kama vile Sierra Leone, Liberia, Visiwa vya Comoro na hata Burundi, ingawa kusema kweli katika nchi zote hizo juhudi za ziada zinahitajika na zinaendelea ili kupata ufumbuzi wa kudumu.

Wengi wenu ni waandishi wa habari na kwa hiyo wafuatiliaji wa makini na karibu wa matukio mbali mbali duniani na hasa katika bara letu. Kwa mantiki hiyo sidhani kuna sababu ya kuwaelezea kwa urefu migogoro mingine kadhaa ambayo hata imekuwa sugu. Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo ni nchi kubwa, yenye utajiri mkubwa na kama ikipata amani na utulivu na kushughulikia maslahi ya watu wake kikamilifu, italeta mabadiliko makubwa sio ya Congo tu bali ya kanda hii yote ya Afrika mashariki, kati na kusini. Kwa sasa, pamoja na juhudi zilizofanyika na makubaliano ya amani yaliyopatikana, nchi hiyo bado haijawa tulivu vya kutosha.

Tunaelewa fika historia ya hivi karibuni ya nchi hiyo, vita vya wenyewe kwa wenyewe na mchango wa baadhi ya nchi za nje zikiwemo za kijirani

zilizozidisha kuzorota kwa hali ya amani na utulivu. Itakumbukwa kwamba wakati mmoja, majeshi ya nchi tano za Kiafrika yalipoingia ndani ya nchi hiyo na kushiriki katika mapambano – Rwanda na Uganda kusaidia waasi na Angola, Namibia na Zimbabwe kusaidia serikali ya Rais Joseph Kabila, aliekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani, Bibi Madeline Albright alivielezea vita vilivyokuwa vinaendelea huko Congo kuwa ni vita vya dunia vya Afrika (*Africa's World War*).

Jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ukivuka mto tu ipo Jamhuri ya Congo (Brazzaville). Nayo ilikumbwa na matatizo makubwa ya vita vya wenyewe kwa wenyewe. Huko, mapambano yaliendeshwa na Viongozi waliotumia majeshi ya mgambo. Kulikuwa na jeshi la mgambo liitwalo NINJA, jengine liitwalo ZULU na jingine liitwalo COBRA. Majeshi yote haya yalikuwa yana silaha za kutosha. Na Jeshi la taifa lenyewe likagawanyika! Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba hata Rais wa Jamhuri wa wakati ule, Bwana Pascal Lissouba naye alitegemea zaidi jeshi lake la mgambo! Nikiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika nilitembelea huko Brazzaville pamoja na kuteua wajumbe maalumu wa kuniwakilisha katika juhudi za kujaribu kuleta suluhisho. Niliwakumbusha Viongozi wa Congo pamoja na Rais wa nchi hiyo zile nasaha za Mwalimu Nyerere kwamba "Nchi inaweza kuwa na vyama vingi vya kisiasa lakini haiwezi kuwa na mfumo wa majeshi mengi" (*A country can have a multiparty system but cannot have a multiarmy system*).

Lipo tatizo kubwa na sugu la Sudan ambako mamilioni ya wananchi wamepoteza roho zao tokea vita vianze upya huko kusini mwa Sudan – vita ambavyo vimeendelea kwa muda wa zaidi ya miaka thelathini. Hivi sasa kuna matumaini makubwa ya kupatikana amani ya kudumu baina ya Serikali ya Sudan na wapiganaji wanaoongozwa na SPLM/SPLA. Lakini pamoja na matumaini hayo, hali ya mustakbal wa amani, utulivu na maendeleo ya Sudan imeathiriwa vibaya sana na matukio ya huko Darfur ambako maelfu ya watu wasiokuwa na hatia

wanaendelea kuuwawa, wengi kujeruhiwa na wengi zaidi kusambaratishwa na kupaswa kuishi maisha ya duni, ya hatari na ya unyonge kama wakimbizi.

Kama kuna nchi moja katika bara letu ambayo watu hawakutegemea kuwa na migogoro ya kikabila ni Somalia. Sote tukiwajua ndugu zetu wa Kisomali kuwa ni watu wenye lugha moja, utamaduni mmoja, wengi wakiwa wa dini moja na madhehebu mamoja na kadhalika. Lakini tokea Rais Siad Barre apinduliwe – zaidi ya miaka kumi na mbili sasa – nchi hiyo imekuwa na vurugu, vita vya wenyewe kwa wenyewe na kutokomeza juhudi mbali mbali zenye lengo la kuleta maelewano na kurejesha amani. Wakati wote huo, nchi hiyo haina serikali kuu. Macho ya Afrika na ya jamii ya kimataifa hivi sasa yanalenga huko Nairobi ambako juhudi zinaendelea kujaribu kuwapatanisha ndugu zetu hao wa Somalia.

Kama nilivyokwisha elezea orodha ni ndefu. Migogoro hii niliyoitaja ndio miongoni mwa ile ambayo imedumu kwa muda mrefu. Ipo mingine. Ningependa kusisitiza pia kwamba zipo baadhi ya nchi ambazo ingawa hivi sasa hazina migogoro inayotajika au vita vya wenyewe kwa wenyewe lakini kwa jinsi ya mambo yanavyokwenda kuna hofu miongoni mwa jamii ya kimataifa ya uwezekano mkubwa migogoro kuzuka na kushamiri katika nchi hizo kama hatua za makusudi hazikuchukuliwa kuzishawishi kuchukua hatua ili kujiepusha na balaa la migogoro.

Kabla sijahitimisha sehemu hii ya hotuba yangu, nitakosea kama sijagusia mgogoro wa Cote d' Ivoire. Hii ni nchi ambayo ilikuwa inatolewa kama mfano kwa utulivu na maendeleo ya kiuchumi na kijamii miongoni mwa nchi zisemazo kifaransa katika Afrika ya Magharibi. Rais wa kwanza wa nchi hiyo, Felix Houphet-Boigny aliweka misingi mizuri ya umoja na mshikamano na kutoachia tofauti za kikabila, kidini au kikanda kushamiri. Pia alikuwa na sera ya nadharia na vitendo ya kuwafanya Waafrika wa nchi mbali mbali za Afrika ya Magharibi wajisikie wapo nyumbani na kwa kufanya hivyo aliitumia vyema nguvu-kazi yao.

Wengi walikaa huko na kuchangia kikamilifu katika maendeleo na uchumi wa nchi hiyo.

Inakisiwa kuwa idadi kubwa miongoni mwa "wageni" hao wameishi katika Cote d' Ivoire zaidi ya miaka thelathini. Wengi wengine wamezaliwa hapo. Inakadiriwa kwamba aslimia arubaini (40%) ya wakazi wa nchi hiyo wana asili ya nchi mbali mbali za Afrika ya Magharibi wakiwemo kutoka Burkina Faso (milioni tatu), Mali (milioni mbili mpaka tatu), Ghana (milioni mbili), Nigeria (milioni moja), Senegal (wasiopungua laki tano) na wengine kutoka Guinea, Benin, Gambia, Mauritania, Niger na Togo. Lakini baada ya kifo cha Rais Houphet-Boigny, ufinyu wa mawazo, uchu wa madaraka na kukataa kukabili ipasavyo changamoto ya demokrasia, imewafanya viongozi wa nchi hiyo kufuata siasa na sera potovu ambazo hatimaye imeingiza nchi hiyo katika vita vya wenyewe kwa wenyewe na kusababisha nchi kugawika sehemu mbili – Kaskazini ambayo hivi sasa inatawaliwa na wapinzani wa Serikali na Kusini ambayo hivi sasa inatawaliwa na Serikali ya nchi hiyo.

Ndugu Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Kuanzia mwanzo wa muongo uliopita, tumeshuhudia kuzuka katika bara letu migogoro inayoteketeza, migogoro ambayo tokea bara letu kuwa huru hatujapata kuiona kwa jinsi ya ukatili na kushamiri kwake, mauaji yaliyokithiri na vurugu zisizo kifani. Tumeshangazwa na tunaendelea kupigwa na butwaa namna gani binadamu anaweza kumfanyia kitendo cha kikatili na cha kinyama binadamu mwenzake na kitu gani hasa kinachomfanya mtu aporomoke kufikia ngazi ya uovu hadi hiyo. Vipi mtu anaweza kuelezea mauaji ya kuangamiza yaliyotokea huko Rwanda? Au mauaji ya maelfu ya wananchi wa Jimbo la Sudan la Darfur? Au vitendo vya waasi wa kule Sierra Leone vya kuwakata viungo mbali mbali watoto wadogo na hata watoto wachanga? Au mauwaji ya Liberia?

Suala la msingi ni kwa nini Afrika katika miaka hii ya karibuni imekuwa midani mikubwa ya migogoro? Pengine si jambo rahisi kuelezea sababu zote zilizosababisha hali hii. Lakini yapo mambo kadhaa ambayo yamechangia hali hii isiyoridhisha. Mambo haya yanaweza kuwa ya kisiasa, ya kikabila, ya kiuchumi, ya kijamii au ya kidini. Ukweli ni kwamba yote haya yanakuwa chanzo cha matatizo na migogoro yanapotumiwa vibaya kwa maslahi ya watu binafsi, au vikundi fulani au jamii na kuwaacha walio wengi nje ya mstari.

Katika Afrika, mojawapo ya vyanzo vikuu vya migogoro ni kutozingatia haki katika mgawanyo wa rasilmali ya nchi na uendeshaji wa dola. Ni jambo lilio wazi kwamba ikiwa haki haitendeki katika utumiaji wa rasilmali ya nchi na ikiwa nguvu za dola zimekusanywa katika mikono ya watu wachache au kikundi au kigenge fulani, na ikiwa haki za watu zinabezwa au hata kukanyagwa, jambo dogo tu linaweza kuwasha moto mkubwa.

Katika suala la haki ningependa kusisitiza umuhimu wa kuheshimu haki za binadamu za watu wetu. Katika historia hakuna waliopata madhila na kuonewa zaidi kwa kunyimwa haki zao za kibinadamu kama Waafrika. Watu wetu walipopigania uhuru walikuwa wanapigania utu wao, heshima zao na haki zao kama binadamu wengine. Vita vya uhuru na ukombozi vilikuwa ni vita vya kutaka kuheshimiwa kwa haki za binadamu na kuleta demokrasia halisi. Kwa hiyo basi ingetegemewa kwamba baada ya uhuru, nchi zetu za Afrika zingekuwa katika mstari wa mbele kabisa kulinda, kuheshimu na kutetea haki hizo. Na la uzito zaidi kuhakikisha kwamba watu wa nchi zetu wanatumia kikamilifu haki zao hizo bila ya vikwazo vyovyote vile na hususan bila ya kuonewa, kuteswa au kuuawa ovyo ovyo.

Ni vyema kukumbushana kuwa nchi zote za Kiafrika zimeridhia na hata kutia saini mikataba mingi kuhusu haki za binadamu; na nchi zote huru za Afrika zimeikubali kikamilifu mikataba miwili muhimu inayohusu haki za binaadamu. Mikataba hiyo ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binaadamu

(Universal Declaration of Human Rights) na Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika kuhusu Haki na Wajibu wa Watu wa Afrika (African Charter on Human and Peoples Rights). Pamoja na hayo yote, baadhi ya nchi zetu au ninaweza kusema kwamba idadi kubwa, kwa namna moja au nyingine haziheshimu kikamilifu mikataba hii na mara nyingine raia wa kawaida wanaendelea kuteseka.

Imeelezwa mara nyingi kuwa umasikini ndio chanzo/sababu ya idadi kubwa zaidi ya migogoro iliyopo katika nchi zinazoendelea. Tokea miaka ya 1980, nchi nyingi za dunia zilizo masikini sana zimekumbwa na migogoro. Lakini hali hii haina maana kuwa migogoro inawakumba masikini tu. Kusema hivyo ni kurahisisha mambo mno. Lakini jambo lisilokuwa na ubishi ni kwamba umasikini unajenga mazingira ya migogoro kuanza. Isitoshe, jambo la hakika ni kuwa migogoro ndio sababu na matukio ya umasikini (impoverishment). Kwa vyovyote vile kuendelea kwa ufukara uliokithiri katika jamii wakati watu wachache au kikundi cha watu wanaishi maisha ya kifahari bila ya kujali wala kubali, kunachangia suitafahamu katika taifa na kunaandaa mazingira ya matatizo na hata migogoro. Ni muhimu sana watu wasifikishwe mahala wakawa hawana matumaini.

Bara letu lina mifano mingi ya wanasiasa waliofilisika ambao hutumia tofauti za kikabila, kikanda au kidini kwa maslahi yao ya muda. Hufanya hivyo kwa lengo la kupata madaraka. Wanadhani kwamba wakishapata kile wanachokipigania yaani uongozi wa dola, basi mambo yanaweza kurejea kama zamani, kabla ya sokomoko waliolichangia kwa kuleta chokochoko za ukabila, udini na ukanda. Wanasahau au kupuuza ule usemi kuwa '*unaweza kulitoa jini kutoka katika chupa lakini huwezi kulirejesha*'. Matukio yake ni kuandaa mazingira ya kupalilia migogoro pamoja na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika baadhi ya nchi zetu.

Ni muhimu pia kutia maanani taathira ya kipindi cha mpito ambacho nchi nyingi za Kiafrika zimekuwa zikikabiliwa nacho. Hapa nakusudia matatizo na

changamoto yatokanayo na kipindi cha mpito kutoka mfumo wa Chama kimoja na uchumi hodhi (Centralised economy) kwenda katika mfumo wa vyama vingi na uchumi huria! Pia ni jambo lilio dhahiri kwamba mara nyingine migogoro ambayo ingeweza kutulizwa na kupatiwa ufumbuzi inaachiwa kuripuka katika mapambano na kuleta maafa makubwa kwa sababu ya uongozi dhaifu, migongano ya kisiasa na matatizo binafsi ya viongozi. Mara nyingine migogoro hii hufanywa ikawa na taathira kubwa zaidi kutokana na vitendo vya nje ya nchi yaani baadhi ya nchi za nje au taasisi zilizopo nje ya Afrika kujiingiza ndani ya mambo ya nchi zetu.

Inaweza kuwa hatujui sababu zote za migogoro hii. Pia hatuwezi kutoa makisio thabiti ya gharama za migogoro hii kwa maana ya taathira kwa binadamu na mali inayoharibiwa. Lakini hatukosei tukisema mamilioni ya roho za watu wetu zimepotea na uharibifu mkubwa wa mali umefanyika. Mamilioni zaidi wamejuruhiwa na miongoni mwao kuwa na vilema vya maisha. Isitoshe migogoro hii imesababisha mamilioni ya watu kuwa wakimbizi nje ya nchi au wakimbizi ndani ya nchi zao wenyewe. Hivi sasa Afrika ina nafasi isiyo ya kujivunia ya kuwa na idadi kubwa ya wakimbizi walioko nje ya nchi na wale "wakimbizi" ambao hawajaweza kupata fursa ya kwenda nje ya nchi lakini wamelazimika kuhama makazi yao na kukimbilia sehemu mbali mbali za nchi yao katika hali ya udhaifu na kusikitisha. Hawa ndio wanaoitwa IDPs (*Internally displaced persons*) Hivi sasa Afrika ina wakimbizi wanaokisiwa kuzidi milioni nne na IDPs wanaokaribia milioni sita.

Takriban nchi zetu zote za Afrika zina matatizo ya namna moja au nyingine ya kiuchumi. Kwa ajili ya umasikini wetu, maendeleo yamekuwa yanakwenda taratibu na mara nyingi taratibu mno. Maendeleo yaliyopatikana, yamewezekana kutokana na kazi kubwa na kujitolea kwa watu wetu. Migogoro inapotokea, maendeleo ya kiuchumi na kijamii yaliyopatikana kwa muda wa miaka mingi husambaratishwa au hata kufutwa kabisa katika muda wa miezi michache, majuma machache, siku chache au hata mara nyingine saa chache.

Kwa mfano mji mzuri wa kupendeza uliokuwa na sifa kem kem wa Brazzaville, Makao Makuu ya Jamhuri ya Congo ulinipa picha sahihi ya uharibifu mkubwa uliofanywa. Wananchi wa Jamhuri ya Congo badala ya kuendelea mbele kuijenga nchi yao na kuleta maendeleo yao wamepaswa kuanza upya kuujenga mji wao. La kusikitisha zaidi ni kwamba ingawa inawezekana kuujenga upya mji kama huo na majengo mengine pamoja na miundo mbinu mbali mbali, haiwezekani kurejesha roho za wale walioteketezwa kwa risasi za bunduki na silaha nyinginezo mbali mbali.

Kama balaa hizo hazitoshi, migogoro hii inapomalizwa inaacha majeraha ambayo ni shida sana kuyatibu/kuyatengeneza. Mengine huwa majeraha ya kudumu. Wanawake, watoto na wazee mara nyingi zaidi huwa ndio wanaoathiriwa. Isitoshe, muda mrefu baada ya bunduki kuwa kimya, vita kumalizika, maafa yanaendelea kuwakumba wananchi wasiokuwa na hatia. Maeneo ya mauaji (*killing fields*) yanaendelea kwa vile mabomu yaliyowekwa ardhini (*Landmines*) yanaendelea kuuwa na kujeruhi watu wetu. Kwa mfano, katika nchi ya Angola inakisiwa kuwa mabomu kama hayo yanayofika milioni kumi yalitegewa. Mabomu hayo yanaendelea kujeruhi wananchi wa nchi hiyo. Ingawa bei ya kila bomu la aina hilo ni rahisi (kama dola tatu za Kimarekani), gharama ya kuyaondoa mabomu hayo ni kubwa (inakisiwa kufika hata dola elfu moja za Kimarekani kwa kila bomu). Ingawa idadi inatafautiana, lakini nchi zilizomo katika migogoro au zilizokuwa katika migogoro kama vile Somalia na Msumbiji zinakabiliwa na tatizo kubwa hilo la *landmines*.

Nchi zetu zinaendelea kuwa na vizazi ambavyo vimekulia katika utamaduni wa mapambano ya silaha na fujo. Tunawezaje kurejesha hali ya kawaida katika mazingira kama hayo? Wale ambao walisababisha mauaji na uharibifu wote huo hawajui kitu chochote kuhusu jinsi ya kurekebisha uharibifu walioufanya. Wanachojua ni jinsi ya kuharibu tu!

Ndugu Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Masuala ya demokrasia na utawala bora ni mambo ya msingi katika kuepukana na majanga ya migogoro na kuleta maendeleo endelevu katika nchi zetu. Uzoefu tulioupata katika muongo uliyopita pamoja na miaka ya hivi karibuni umedhihirisha kuwa amani, usalama na utulivu, maendeleo, ushirikiano, usawa, heshima (*dignity*) na masikilizano itabakia ndoto kama hakuna utawala bora. Kwa upande mwingine, demokrasia na utawala bora unahikikisha ushirikishwaji wa dhati wa wananchi katika midani ya siasa, uchumi na maendeleo ya jamii katika nchi zetu.

Ninapozungumzia mfumo wa demokrasia nakusudia mfumo wa utawala ambao unawapa uwezo wananchi kuchagua viongozi wao kila baada ya kipindi kinachojulikana katika chaguzi ambazo ni huru na za haki. Kwa kufafanua zaidi demokrasia ni mfumo wa utawala ambao wananchi wanaamua nani awe kiongozi/viongozi wao, na kwa kipindi gani. Lakini ni muhimu kusisitiza kwamba demokrasi na utawala bora hauji kwa kuwa na chaguzi huru tu. Ni muhimu kujenga na kuendeleza taasisi mbali mbali ambazo ndio zinazohimili mfumo huo. Pia kwa Katiba imara, mahakama huru, utawala wa sheria, vyombo vya habari vilivyo huru, jumuiya imara za wananchi, viongozi walio waadilifu, wenye kuwasikiliza wananchi na walio karibu nao, na wananchi wenye muamko na walio wepesi wa kukemea na kuzuia maovu yanapotendeka.

Wakati huo huo inaeleweka kuwa demokrasia na utawala bora si jambo linalokuja kwa mkupuo. Ni mchakato unaochukua muda ukihusisha maeneo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ndio maana katika midani ya kitaifa na Bara letu kumekuwa na utashi wa kupanua wigo wa kisiasa, kulinda haki za binadamu, kuimarisha utawala wa kisheria, kuendeleza na kuimarisha utamaduni wa kuvumiliana na kuendeleza ufanisi na uongozaji thabiti wa uchumi.

Katika miaka kumi na mitano iliyopita, takriban nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikichukua hatua kuendeleza taasisi zao za kidemokrasi na utendaji wa kazi, zimefanya mageuzi katika utumishi wa Serikali na mashirika ya umma pamoja na kufanya mabadiliko katika vyombo vya kuendesha mambo. Vikundi vya kiraia (*civil society*) vimekuwa imara zaidi na sekta binafsi inazidi kutoa mchango wake katika maendeleo ya nchi za Afrika.

Ndugu waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Vugu vugu la kupigania Uhuru katika bara letu lilikuwa pia ni vugu vugu la kuleta amani na haki. Kwa hiyo watu wetu wakiwa hawana amani, uhuru wao utakuwa umepata ufa mkubwa. Kielelezo kimoja kinachoonyesha kinaganaga ukweli huu ni suala la wakimbizi katika Afrika. Miaka thelathini na tano (35) iliyopita Afrika ilikuwa na wakimbizi laki sita. Leo kama nilivyokwisha elezea hapo mapema tunazungumzia wakimbizi zaidi ya milioni nne na wale wakimbizi waliolazimika kuhama makwao na kusambaa au kusambazwa sehemu mbali mbali za nchi zao (IDPs) wanaokaribia milioni sita. Kwa watu hawa ambao wamelazimishwa kuishi maisha yasiyokuwa na matumaini, na kwa wale wengi ambao wamepoteza njia za kujipatia maisha na kushuhudia balaa la vifo vya familia zao, watoto wao, ndugu zao au jamaa zao, Uhuru unakuwa ni jambo lisilokuwa na maana sana. Changamoto kubwa ya kutanzua migogoro na kuleta amani katika vita vya wenyewe kwa wenyewe ni kuwapa watu hawa matumaini na kuimarisha maana na thamani ya Uhuru katika bara letu.

Changamoto ya kuleta amani katika migogoro ya ndani ya nchi ni kwanza kabisa kujitahidi kuepusha mgogoro usitokee. Ili kufanya hivyo, nchi zetu zinapaswa kuwa na sera na kujenga tabia ya vitendo na imani ambazo hazilengi kuleta mgogoro. Hapa nakusudia kwamba nchi zetu ziwe na sera na utaratibu ambao watu wanahisi wameshirikishwa na ambazo zinalenga kuleta usawa (*equity*) na haki katika jamii. Mara nyingi tumeshuhudia katika baadhi ya nchi

zetu za Afrika jamii zetu zikigawanyika kutokana na mapambano ya ndani kwa ndani ya kupata nafasi sawa ya fursa, rasilmali za taifa na kushiriki katika mchakato wa kisiasa. Siasa za kutojali mawazo ya wengine au kuitenga sehemu ya jamii (*Politics of rigidity and exclusion*), zimekuwa vyanzo vya matatizo (*hotbeds of tension*) kama vile zinavyofanya siasa za ukabila, ukanda na ukosefu wa uvumilivu katika mambo ya dini.

Ili Afrika iondokane kabisa na urithi wa siasa zinazoleta mgawanyiko na migogoro, lazima tuwe tayari kujenga utamaduni mpya wa kisiasa – utamaduni unaoleta maelewano na umoja na ambao umeasisiwa katika misingi ya usawa (*equity*), haki na kuvumiliana na kuheshimiana. Katika miaka ya hivi karibuni na hadi sasa bara letu limekuwa likipitia katika kipindi cha mabadiliko makubwa. Kisiasa tunaona kuwa nchi nyingi zinafuata mfumo wa vyama vingi vya kisiasa (*political pluralism*) na kuwa na chaguzi ambazo zinashirikisha vyama vingi badala ya kuwa na chama kimoja kama ilivyokuwa hapo zamani. Kiuchumi bara zima kwa jumla limekuwa na harakati za kufanya mageuzi na kujiandaa kukabiliana na hali halisi ya hivi sasa (*Restructurinng and adjusting*).

Haya yote yanafanywa kwa madhumuni makuu ya kuleta mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi ambayo yataweza kudumisha na kuendeleza jamii zetu katika miaka ijayo. Kwa hiyo changamoto inayotukabili ni jinsi gani ya kudhibiti kipindi hichi cha mpito. Kisiasa, tujitahidi kuhakikisha kwamba mabadiliko haya yanafanyika kwa utaratibu mzuri (*smoothly*) bila ya kuathiri vibaya mafanikio mengi ya kisiasa na kiuchumi ambayo yalipatikana kwa gharama kubwa. NDIYO, TUNAHITAJI KUBADILI JINSI TUNAVYOENDESHA MAMBO YETU YA KISIASA KATIKA AFRIKA.

Lazima tuhakikishe kuwa kuna ushirikishwaji mkubwa zaidi wa watu wetu katika mchakato wa utawala. Ni muhimu kwa viongozi wetu kuhakikisha kwamba serikali zetu katika Afrika zinawajibika na harakati zake ziko wazi. Haki za binadamu zinaheshimiwa na kuendelezwa. Na katika upeo huo ni muhimu

vyombo vya habari vikawa na uhuru kamili wa kujieleza. Lakini hapo hapo kwa vile ninazungumza katika Kongamano lililotayarishwa na waandishi wa habari, naamini ni wajibu wangu kukumbusha kwamba nanyi mna dhamana na jukumu kubwa la kuhakikisha mnawajibika na mnayoandika. Ni muhimu kuwa na Mahakama ambazo ni huru na zinazohakikisha kwamba haki inatendeka na inaonekana kutendeka. Hii ndio baadhi ya misingi ya kidemokrasia ambayo inakubalika na kuthaminiwa kimataifa. Lakini hapo hapo tunawajibika kuhakisha kwamba mchakato wa kujenga demokrasia unaendeshwa kwa amani na kwa njia ambayo inazingatia hali halisi ya nchi zetu. Vivyo hivyo, demokrasia tunayotaka kuijenga na/au kuiimarisha lazima izingatie mahitaji maalumu ya jamii zetu na itilie maanani mila zetu, utamaduni wetu na historia ya nchi zetu.

Nimeona ni vyema nisisitize jambo moja la ziada kuhusu mchango wa vyombo vya habari. Sote tunaelewa fika kwamba vyombo hivi – ikiwa ni magazeti, radio na televisheni – vinaweza kusaidia sana katika ujenzi na maendeleo ya nchi zetu na bara letu. Vina wajibu kukosoa pale penye dosari na kutahadharisha pale mambo yanapokwenda kombo au kuhatarisha kusambaratika kwa maadili ya mataifa yetu. Wakati huo huo tunao uzoefu wa kutosha katika Afrika kutambua kwamba kama vile vyombo vya habari vinavyoweza kusaidia kujenga na kuwa chachu ya maendeleo na mageuzi muwafaka, lakini vikitumika vibaya, uwezo wake wa kubomoa na kuchafua hauna kikomo. Na vikifanya hivyo, mara nyingine athari yake huwa ni maafa na majanga makubwa kwa jamii. Kwa mfano, sote tunakumbuka jinsi Radio huko Rwanda – Radio Mille Colline ilivyotumika kuchochea na kuendeleza mauaji ya halaiki ya kikatili katika nchi hiyo mwaka 1994. Hii inatokana na ukweli kwamba watu wetu wengi wanaamini kabisa yale yanayoandikwa katika magazeti, au kusomwa katika radio na televisheni.

Ndugu Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Ningependa kumalizia kwa kusisitiza mambo mawili. Kwanza, pamoja na juhudi zinazofanywa na nchi zetu mbali mbali katika kukabiliana na migogoro na kutanua demokrasia na utawala bora, ni wazi kuwa juhudi hizi zitapata mafanikio makubwa zaidi zikiunganisha umoja na mshikamano wa nchi zetu zote Afrika. Na ndio maana Umoja wa Afrika (AU) na kabla yake Umoja wa Nchi za Afrika (OAU) umetoa umuhimu wa pekee wa mambo haya. Katiba (*Constitutive Act*) ya AU imepanua zaidi uwezekano wa Umoja huo kuchukua hatua zipasazo kukabiliana na balaa la migogoro pamoja na hivi sasa kukiimarisha kile chombo kilichokuwa kikishughulikia migogoro katika bara letu. Baraza la Amani na Usalama la AU ambalo lilizinduliwa rasmi huko Addis Ababa tarehe 25 Mei, mwaka huu wa 2004 ni kielelezo tosha kwamba nchi zetu zimepania kukabiliana na tatizo hili sugu na ambalo mara nyingi linaaibisha na kudhalilisha bara letu. Ni wazi kuwa kuna mengi ambayo yanahitajika kufanyika pamoja na kuupatia Umoja wa Afrika nyenzo na fedha za kutekeleza maamuzi yake. Lakini hatua iliyofikiwa ni ya kutia moyo.

Jambo la pili ni kusisitiza umuhimu wa kujifunza yanayotokea katika nchi mbali mbali za bara letu. Ili tuendelee kudumisha amani, usalama na utulivu katika taifa letu – mambo ambayo ni ya msingi kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wetu, ni muhimu kujiepusha na makosa ambayo yamefanyika katika baadhi ya nchi hizo na kuzaa matatizo ambayo baadaye yakawa migogoro. Kama walivyosema wahenga: Usipoziba nyufa utajenga ukuta. Kwa vyoyote vile, ngao kubwa ya taifa letu ni umoja, mshikamano na uelewano miongoni mwa jamii yetu licha ya tofauti ya misimamo ya kisiasa.

Ndugu Viongozi na wanachama wa **Zanzibar Press Club**,
Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Nguvu ya pamoja ya Waafrika kuandaa na kupanga mustakbal wa bara letu hivi sasa ni kubwa kuliko hapo zamani, tukizingatia uzoefu mchungu tuliopitia ikiwa ni Angola, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jamhuri ya

Congo, Central African Republic, Cote d'Ivoire, Rwanda, Somalia, Sudan, Liberia, Sierra Leone au Uganda. Haja ya kuitumia nguvu hii ina uzito zaidi sasa kuliko wakati wowote ule wa zamani. Kuihamasisha nguvu hiyo ili kuyafanya maisha ya watu wetu katika karne ya ishirini na moja, yawe ya kustahamilika zaidi, yenye kuwezekana zaidi, yenye demokrasia zaidi, yenye usalama zaidi na yaliyo endelevu zaidi ndio mambo yanayohitajika kuiwezesha Afrika kuchukua nafasi yake ipasavyo katika jamii ya kimataifa chini ya misingi ya uelewano wa kimataifa na kuchukua majukumu ya pamoja.

Nimearifiwa kwamba shughuli hii ni 'kutoka ukumbi' kwa **Zanzibar Press Club**. Ni matumaini yangu kwamba shughuli kama hizi za kujadili na kubadilishana mawazo kuhusu mustakabali wa taifa letu, matatizo na mafanikio ya bara letu la Afrika, na mwenendo wa dunia zitakuzwa na kuendelezwa. Hii ni njia moja wapo ya kujielimisha na kuelimishana, na ili tuweze kutowa mchango mkubwa zaidi kwa jamii. Kama mwanahabari mwenzenu, napenda pia kushauri kwamba tuwe tunaadhimisha siku ya vyombo vya habari duniani (*World Press Day*), na tuitumie kwa kukuwakumbuka na kuwaenzi wenzetu ambao wametowa mchango mkubwa katika fani hii hapa nchini. Napenda tena kuwashukuru viongozi na wanachama wa **Zanzibar Press Club** kwa mualiko huu.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.